OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, JANUARI, MWAKA 2024

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 22 zimeripotiwa mwezi wa Januari, 2024. Wilaya ya Kaskazini "B", Kati na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya sawa na asilimia 18.2 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Januari 2024**




Idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Januari, 2024 zimeongezeka kwa asilimia 4.8 kufikia ajali 22 kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka ajali 21 kwa mwezi wa Disemba 2023

Kwa mwezi wa Januari 2024, wilaya ya Kasazini "B", Kati na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi nne (4) kwa kila wilaya na wilaya ya Kaskazini "B" iliripotiwa kuwa na ajali zaidi tano (5) kwa mwezi wa Disemba 2023.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 22.2 na kufikia ajali 22 kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka ajali 18 kwa mwezi wa Januari 2023.


Kwa mwezi wa Januari 2024, wilaya ya Kaskazini "B", Kati na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali nne (4) kwa kila wilaya na Januari 2023 wilaya ya Kati ilikuwa na ajali zaidi, nane (8).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Januari 2023 na Januari 2024**





Jumla ya waathirika 40 wameripotiwa mwezi wa Januari, 2024, ambapo waathirika wote walikuwa wanaume. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 11 sawa na asilimia 27.5 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Januari 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Januari 2024 wamepungua kwa asilimia 38.1 kufikia waathirika 13 waliofariki kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka waathirika 21 waliofariki kwa mwezi wa Disemba 2023.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wameongezeka kwa asilimia 22.7 na kufikia waathirika 27 waliojeruhiwa mwezi wa Januari, 2024 kutoka waathirika 22 waliojeruhiwa kwa mwezi wa Disemba, 2023.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi wa Januari 2024 wamepungua hadi kufikia waathirika 13 kutoka waathirika 15 waliofariki kwa mwezi wa Januari 2023.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Januari 2023 na Januari 2024**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi wa Januari 2024 wameongezeka kwa asilimia 17.4 kufikia waathirika 27 kutoka waathirika 23 waliojeruhiwa mwezi wa Januari 2023.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Januari 2023 na Januari 2024**




Mwezi wa Januari, 2024 waathirika wengi walikuwa abiria (waathirika 15). Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki); wapanda baiskeli na pikipiki walikuwa kumi na tatu (13), waenda kwa miguu tisa (9) na madereva walikuwa watatu (3).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Januari 2024**





Kwa mwezi wa Januari 2024, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 09:01 - 12:00 jioni ambapo zimeripotiwa kutokea ajali saba (7).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Januari 2024**




Jumla ya ajali 22 zilizoripotiwa mwezi wa Januari, 2024, ajali 18 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali 3 zimesababishwa na uzembe wa madereva na ajali 1 imesababishwa na hitilafu ya umeme. Mkoa wa Kaskazini Unguja unaongoza kwa kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 6).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Januari 2024**.





***KUMBUKA:Sababu ya hitilafu ya umeme ni hali ya gari kuwaka moto(kuripuka) inayosababishwa na nyaya za umeme ndani ya gari.***

## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa **2,174** yameripotiwa mwezi wa Januari 2024, ambapo makosa **2,167** yameripotiwa kwa wanaume na makosa **saba (7)** yameripotiwa kwa wanawake.


Wilaya ya Magharibi "A" ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa **490**) sawa na asilimia **22.5** kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 35 (asilimia 1.6) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.

**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Januari 2024**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Januari 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (**makosa 974**) yakifuatia Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (**makosa 443**) na Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva wa gari za abiria (**makosa 261).** Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya makosa yote tisa (9) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 77.2


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Januari 2024**



Idadi ya makosa kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 33.4 na kufikia makosa 2,174 kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka makosa 3,264 mwezi wa Disemba 2023.

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Januari 2024 (Makosa 490) na wilaya ya Magharibi "B" ilikuwa na idadi kubwa ya makosa kwa mwezi wa Disemba 2023 (makosa 625).


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**




Idadi ya makosa kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 10.7 na kufikia makosa 2,174 kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka makosa 2,434 kwa mwezi wa Januari 2023.

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Januari 2024 (makosa 490) na mwezi wa Januari, 2023 wilaya ya Magharibi 'B' iliongoza kwa makosa ya barabarani (makosa 450).

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Januari 2023 na Januari 2024**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 22 zimeripotiwa mwezi wa Januari, 2024. Wilaya ya Kaskazini "B", Kati na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya sawa na asilimia 18.2 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

Mlinganisho wa idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Januari, 2024 zimeongezeka kwa asilimia 4.8 kufikia ajali 22 kwa mwezi wa Januari 2024 kutoka ajali 21 kwa mwezi wa Disemba 2023

Jumla ya makosa **2,174** yameripotiwa mwezi wa Januari 2024, ambapo makosa **2,167** yameripotiwa kwa wanaume na makosa **saba (7)** yameripotiwa kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Januari 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (**makosa 974**) sawa na asilimia 44.8 ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Januari 2024**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 3 | 13.6 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 3 | 0 | 3 | 11.1 | 5 | 0 | 5 | 12.5 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 18.2 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 9 | 0 | 9 | 33.3 | 11 | 0 | 11 | 27.5 |
| Kati | 4 | 18.2 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 1 | 0 | 1 | 3.7 | 3 | 0 | 3 | 7.5 |
| Kusini | 2 | 9.1 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 4 | 0 | 4 | 14.8 | 4 | 0 | 4 | 10.0 |
| Mjini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 9.1 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 3 | 0 | 3 | 11.1 | 5 | 0 | 5 | 12.5 |
| Magharibi 'B' | 4 | 18.2 | 4 | 0 | 4 | 30.8 | 1 | 0 | 1 | 3.7 | 5 | 0 | 5 | 12.5 |
| Wete | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Micheweni | 1 | 4.5 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 3.7 | 1 | 0 | 1 | 2.5 |
| Chake chake | 1 | 4.5 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 7.4 | 2 | 0 | 2 | 5.0 |
| Mkoani | 1 | 4.5 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 3 | 0 | 3 | 11.1 | 4 | 0 | 4 | 10.0 |
| **Zanzibar** | **22** | **100** | **13** | **0** | **13** | **100** | **27** | **0** | **27** | **100** | **40** | **0** | **40** | **100** |

## Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Januari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **22** | **1** | **0** | **1** | **2** | **0** | 2 | **1** | **0** | **1** | **12** | **0** | **12** | **7** | **0** | **7** | **8** | **0** | **8** | **4** | **0** | **4** | **5** | **0** | **5** |

### Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 | Dis-23 | Jan-24 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 3 | 0 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 4 | 11 | 9 | 7 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 10 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kati | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 2 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 2 | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 4 | 2 | 1 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 4 | 0 | 7 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **21** | **22** | **22** | **27** | **21** | **13** | **4** | **2** | **0** | **1** | **16** | **12** | **3** | **1** | **1** | **8** | **12** | **7** | **1** | **5** | **6** | **4** |

## Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Januari 2023 na Januari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 | Jan 2023 | Jan 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 4 | 18 | 9 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 15 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 8 | 4 | 3 | 1 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 2 | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 4 | 0 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **18** | **22** | **23** | **27** | **15** | **13** | **2** | **2** | **1** | **1** | **20** | **12** | **0** | **1** | **0** | **8** | **12** | **7** | **1** | **5** | **2** | **4** |

## Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Januari 2024

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 10 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 35 | 0 | 35 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 10 | 0 | 10 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 103 | 0 | 103 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 76 | 0 | 76 | 12 | 0 | 12 | 7 | 0 | 7 | 75 | 0 | 75 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 24 | 0 | 24 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 34 | 0 | 34 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 94 | 0 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 27 | 0 | 27 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 13 | 0 | 13 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 20 | 3 | 23 | 24 | 0 | 24 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 4 | 14 | 0 | 0 | 0 | 27 | 0 | 27 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **11** | **0** | **11** | **137** | **4** | **141** | **322** | **5** | **327** | **644** | **3** | **647** | **443** | **0** | **443** |

### Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Januari 2024

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 | 19 | 97 | 0 | 97 | 0 | 0 | 0 | 186 | 0 | 186 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 0 | 44 | 209 | 0 | 209 | 0 | 0 | 0 | 377 | 0 | 377 |
| Kati | 11 | 0 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 58 | 0 | 58 | 0 | 0 | 0 | 268 | 0 | 268 |
| Kusini | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 41 | 0 | 41 | 65 | 0 | 65 | 15 | 0 | 15 | 164 | 0 | 164 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 55 | 0 | 55 | 102 | 0 | 102 | 0 | 0 | 0 | 259 | 0 | 259 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 41 | 0 | 41 | 316 | 0 | 316 | 0 | 0 | 0 | 490 | 0 | 490 |
| Magharibi 'B' | 14 | 0 | 14 | 0 | 0 | 0 | 21 | 0 | 21 | 101 | 0 | 101 | 0 | 0 | 0 | 173 | 0 | 173 |
| Wete | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 50 | 0 | 50 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 35 | 0 | 35 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 12 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 | 67 | 3 | 70 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 10 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 98 | 4 | 102 |
| **Zanzibar** | **31** | **0** | **31** | **0** | **0** | **0** | **261** | **0** | **261** | **974** | **0** | **974** | **22** | **0** | **22** | **2,167** | **7** | **2,174** |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Januari, 2023 na Januari, 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Januari 2023 | Januari 2024 | Januari 2023 | Januari 2024 | Januari 2023 | Januari 2024 | Januari 2023 | Januari 2024 | Januari 2023 | Januari 2024 | Januari 2023 | Januari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 4 | 2 | 13 | 10 | 5 | 0 | 60 | 23 | 34 | 35 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 2 | 2 | 17 | 10 | 6 | 1 | 92 | 8 | 83 | 103 |
| Kati | 0 | 0 | 3 | 7 | 78 | 76 | 103 | 12 | 117 | 29 | 79 | 75 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 26 | 6 | 31 | 10 | 32 | 24 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 34 | 64 | 49 | 34 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 62 | 2 | 107 | 37 | 0 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 74 | 0 | 106 | 10 | 123 | 27 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 5 | 0 | 44 | 20 | 22 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 2 | 2 | 15 | 12 | 16 | 13 |
| Chake chake | 0 | 0 | 1 | 1 | 21 | 23 | 20 | 24 | 24 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 14 | 17 | 34 | 19 | 27 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **11** | **12** | **141** | **119** | **327** | **65** | **647** | **247** | **457** | **443** |

**Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Januari, 2023 na Januari, 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Kutofunga Namba mbele ya Chombo cha Moto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 | Januari 2022 | Januari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 19 | 154 | 97 | 0 | 0 | 301 | 186 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 44 | 187 | 209 | 10 | 0 | 432 | 377 | 0 | 0 |
| Kati | 7 | 11 | 0 | 0 | 52 | 0 | 42 | 58 | 7 | 0 | 488 | 268 | 7 | 11 |
| Kusini | 4 | 3 | 13 | 0 | 30 | 41 | 45 | 65 | 0 | 15 | 187 | 164 | 4 | 3 |
| Mjini | 35 | 0 | 0 | 0 | 32 | 55 | 223 | 102 | 0 | 0 | 373 | 259 | 35 | 0 |
| Magharibi 'A' | 141 | 0 | 0 | 0 | 23 | 41 | 202 | 316 | 0 | 0 | 535 | 490 | 141 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 14 | 0 | 0 | 43 | 21 | 279 | 101 | 0 | 0 | 625 | 173 | 0 | 14 |
| Wete | 0 | 3 | 0 | 0 | 5 | 9 | 18 | 0 | 0 | 7 | 97 | 50 | 0 | 3 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 6 | 4 | 0 | 0 | 45 | 35 | 0 | 0 |
| Chake chake | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 11 | 12 | 0 | 0 | 91 | 70 | 14 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 17 | 18 | 10 | 0 | 0 | 90 | 102 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **201** | **31** | **13** | **0** | **265** | **261** | **1,185** | **974** | **17** | **22** | **3,264** | **2,174** | **201** | **31** |

**Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 10 | 5 | 0 | 28 | 23 | 78 | 35 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 3 | 2 | 2 | 10 | 3 | 1 | 25 | 8 | 83 | 103 |
| Kati | 0 | 0 | 27 | 7 | 130 | 76 | 31 | 12 | 37 | 29 | 100 | 75 |
| Kusini | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 20 | 6 | 23 | 10 | 24 | 24 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 68 | 4 | 175 | 64 | 25 | 34 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 94 | 2 | 112 | 37 | 17 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 107 | 0 | 218 | 10 | 35 | 27 |
| Wete | 0 | 0 | 3 | 0 | 8 | 0 | 10 | 0 | 38 | 20 | 13 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 19 | 12 | 28 | 13 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 23 | 17 | 24 | 17 | 0 | 14 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 14 | 22 | 34 | 34 | 27 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **40** | **12** | **142** | **119** | **368** | **65** | **714** | **247** | **451** | **443** |


**Inaendelea… Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Disemba 2023 na Januari 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 | Disemba 2023 | Januari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 38 | 19 | 89 | 97 | 0 | 0 | 243 | 186 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 44 | 91 | 209 | 0 | 0 | 230 | 377 |
| Kati | 22 | 11 | 0 | 0 | 52 | 0 | 37 | 58 | 0 | 0 | 436 | 268 |
| Kusini | 0 | 3 | 18 | 0 | 0 | 41 | 15 | 65 | 0 | 15 | 105 | 164 |
| Mjini | 0 | 0 | 23 | 0 | 0 | 55 | 50 | 102 | 0 | 0 | 341 | 259 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 21 | 41 | 57 | 316 | 0 | 0 | 301 | 490 |
| Magharibi 'B' | 0 | 14 | 27 | 0 | 0 | 21 | 63 | 101 | 0 | 0 | 450 | 173 |
| Wete | 0 | 3 | 0 | 0 | 7 | 9 | 12 | 0 | 0 | 7 | 91 | 50 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 5 | 4 | 0 | 0 | 55 | 35 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 10 | 17 | 12 | 0 | 0 | 74 | 70 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 21 | 17 | 20 | 10 | 0 | 0 | 108 | 102 |
| **Zanzibar** | **23** | **31** | **68** | **0** | **172** | **261** | **456** | **974** | **0** | **22** | 2,434 | **2,174** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Januari 2024**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 186 | 4,223,000 |
| Kaskazini 'B' | 377 | 8,666,000 |
| Kati | 237 | 5,456,500 |
| Kusini | 160 | 3,680,000 |
| Mjini | 232 | 5,701,500 |
| Magharibi 'A' | 490 | 11,940,000 |
| Magharibi 'B' | 172 | 8,004,000 |
| Wete | 50 | 1,127,000 |
| Micheweni | 35 | 759,000 |
| Chake chake | 95 | 2,257,000 |
| Mkoani | 82 | 1,950,000 |
| **Zanzibar** | **2,116** | **53,764,000** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Januari 2024**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Januari 2024**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar